



BODI YA MAPATO ZANZIBAR **TAARIFA KWA UMMA**

MAKUSANYO YA KODI YA ROBO YA PILI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (OKTOBA- DISEMBA, 2022)

Zanzibar, 01 Januari, 2023:

Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), inawatangazia Wananchi wote wa Zanzibar kwamba katika kipindi cha Robo ya pili ya Mwaka wa Fedha, 2022/2023, yaani Oktoba - Disemba, 2022, ilipaswa kukusanya **Tshs. 154.922 bilioni**, na **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs. 154.299 bilioni**, ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 99.6** wa Makusanyo ya Kodi tarajiwa, sawa na Makusanyo ya wastani wa **Tshs 51.433 bilioni** kwa mwezi.

Aidha, Makusanyo halisi ya Robo ya Pili ya mwaka huu, yanaonesha **UKUAJI Mkubwa wa Makusanyo halisi wa asilimia 76.92**, yakilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka uliopita wa 2021/2022, yaliyokuwa **Tshs. 87.216 bilioni**. Jedwali Na. 1 linatoa ufafanuzi zaidi.

Kipekee, kwa Mwezi Novemba, 2022, ZRB, ilifanikiwa kukusanya **Tshs.55.931 bilioni**, kati ya lengo la **Tshs. 53.269 bilioni**, ambao ni **Ufanisi mkubwa zaidi wa asilimia 105**.

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato katika Robo ya Pili ya Mwaka 2022/2023

Mwezi	2021/22	2022/2023		Ufanisi	Ukuaji
	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)	Makisio	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)		
Oktoba	27.908	50.189	48.682	97.00%	74.44%
Novemba	30.215	53.269	55.931	105.00%	85.11%
Disemba	29.093	51.464	49.686	96.55%	70.78%
Jumla	87.216	154.922	154.299	99.60%	76.92%

Ukuaji wa Makusanyo ya Kodi wa zaidi ya asilimia **76.92%**, UNATHIBITISHA KUONGEZEKA Uwajibikaji wa Ulipaji Kodi wa Hiari miongoni mwa Walipakodi, Pamoja na Ufanisi wa ZRB. Aidha, ni Uthibitisho wa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar na kuwepo kwa Sera nzuri za Uwekezaji.



Kwa Heshima na Unyenyekevu Mkubwa, **TUNAWAPONGEZA** sana Walipakodi wote kwa **Kutimiza Wajibu wao wa Kiraia wa Kulipa Kodi kwa Hiari.**

Kwa Muktadha huo, ZRB, imefanikiwa katika **kipindi cha miezi sita ya mwaka wa Fedha 2022/2023, kukusanya jumla ya Tsh 286.093 bilioni** sawa na **asilimia 98.64** ya lengo la kukusanya **Tsh 290.048 bilioni.**

Aidha, ZRB, inatoa pongezi za dhati kwa **Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** na viongozi wote wa Serikali chini ya usimamizi wa Waziri wa Nchi (OR), Fedha na Mipango, kwa **Uhamasishaji na Miongozo** yao inayo rahisisha sana Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi. **Kipekee, ninawapongeza Watumishi Wazuri wa ZRB, ambao wanatimiza wajibu wao kwa Jitihada kubwa sana kuhakikisha tunafanikiwa.**

Katika kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi katika Robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, ZRB, itaendelea kufanya yafuatayo:

1. Kuwataka Wananchi Kuendelea **Kudai Risiti za Kielektroniki kila wanapofanya manunuzi, na Kuwataka wafanyabiashara kutoa Risiti za Kielektroniki kila wanapofanya Mauzo.** Pia, Kuchukua Hatua za Kisheria kwa Wafanyabiashara wakubwa ambao hawajaunganisha (Integration) Mifumo yao na Mfumo wa VFMS, **hususan wafanyabiashara wa HOTELI na Makampuni Makubwa.**
2. Kuboresha Huduma kwa Walipa Kodi, ambao kwetu ni Washirika muhimu (Partners), kwa Kuimarisha Huduma za Ofisi za Mikoa, ikiwemo **kuchukua Hatua Stahiki dhidi ya Watumishi wetu** watakaokwenda kinyume na Maadili ya Kazi ikiwemo kutotoa huduma bora na lugha zinazokubalika (Customer care) kwa Walipakodi,
3. Kuchukua hatua za Kisheria kwa mawakala wote wa Kodi, wakiwemo Taasisi za Serikali (Withholding Tax Agents) wasiowajibika kulipa Kodi WANAZOZUIA kwa Makusudi, ikiwemo kuwatoza Adhabu na Riba stahiki,
4. Kuanza Matumizi ya MFUMO MPYA wa Usimamizi na Ukusanyaji Mapato ya Kodi (**ZIDRAS- Zanzibar Integrated Domestic Revenue Administration System**), ambao utauganishwa na Mifumo mingine ikiwemo mfumo wa ZANMALIPO, UHAMIAJI, BPRA na TANCISS).

ZRB inawashukuru sana Walipakodi wote kwa kulipa kodi kwa HIARI Mwaka 2022, na **KUWATAKIA HERI YA MWAKA MPYA 2023,** Pamoja na Kuwahakikishia Ushirikiano Mkubwa katika Kurahisisha Biashara zao.

"Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar"


Yusuph Juma Mwenda
KAMISHNA



Zanzibar_Revenue_board

2